# JARIDA LA MWEZI

TOLEO NA. 008


AGOSTI, 2021

TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY




## 1 BODI YAWATAKA WADAU KUTOA USHIRIKIANO MZURI TMA

## 2 DKT. KIJAZI AELEZA FAIDA KWA NCHI WANACHAMA WA WMO



## 3 FAHAMU ZAIDI: MASUALA MUHIMU YA KUZINGATIA KATIKA UTABIRI WA BAHARINI



## KITAIFA

# BODI YAWATAKA WADAU WA HALI YA HEWA KUTOA USHIRIKIANO MZURI KWA TMA

**Dar es Salaam**



"Ili taarifa hizi za utabiri zilizoandaliwa kwa kila wilaya, ziwe na tija iliyokusudiwatunahitajikuipatia Mamlaka ushirikiano mzuri katika kuhakikisha taarifahizizinawafikiawatumiajiwamwisho kwenye sekta mbalimbali ili kuchangia ukuaji wa uchumi hapa nchini", Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), Dkt. Makame O. Makame alisisitiza hayo wakati akifungua rasmi mkutano wa wadau wa utabiri wa msimu wa mvua za vuli (Oktoba hadi Disemba) 2021 uliofanyika katika ukumbi wa mikutano wa 'Law School', Dar es Salaam.

Aidha, Dkt. Makame aliendelea kusisitiza kuwa taarifa za hali ya hewa zinalenga kusaidia nchi kufikia malengo ya Mpango wa Taifa katika kujenga uchumi wa viwanda katika eneo la uzalishaji mazao ya chakula na biashara, nishati na maji. Alisema huduma za hali ya hewa zikitumika ipasavyo zitasaidia upatikanaji wa malighafi na nishati kwa viwanda hapa nchini.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa

Mamlaka ya hali ya hewa Tanzania Dkt. Agnes Kijazi amesema kuwa Mkutano huu ni muhimu sana kwa wataalam wa hali ya hewa katika kujifunza kwa undani na kuongeza uelewa wa matumizi sahihi ya taarifa za hali ya hewa katika sekta mbalimbali na hivyo kuendelea kuboresha taarifa zinazotolewa na Mamlaka.

Aidha Dkt. Kijazi aliwakumbusha wadau kuwa TMA inaendelea kufanya utafiti kujua mwenendo wa mvua za mawe zilizojitokeza hivi karibuni katika baadhi ya maeneo hapa nchini, ambapo utafiti huo utasaidia kuboresha utabiri ili kupunguza au kuepusha athari zitokanazo na mvua hizo za mawe.

Pia wadau walioshiriki katika mkutano huo wameipongeza Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) kwa juhudi kubwa wanazozifanya katika kutoa taarifa zilizo sahihi na kwa wakati ambazo wanazitumia katika utekelezaji wa mipango ya sekta zao.

Sekta ambazo zilipata fursa ya kuchangia jinsi walivyoutumia utabiri wa Masika (Machi hadi Mei, 2021) ni pamoja na; Sekta ya Kilimo ambao walisema mazao ya mizizi yaliendelea vizuri katika msimu husika. Sekta ya Maafa walielezea namna utabiri ulivyoleta ufanisi katika njia za kukabiliana na maafa na hivyo kupunguza maafa, Sekta ya afya ambao walisema utabiri ulitumika kwa manufaa katika sekta hiyo. Kwa upande wa Sekta ya Mifugo walisema, miundo mbinu ya ufugaji iliboreshwa ili kukabiliana na athari ambazo zingeweza kujitokeza na Sekta ya Nishati kwa upande wa tafiti za mafuta walisema miradi ya tafiti hizo inaendelea kutumia taarifa za hali ya hewa.



## KIMATAIFA

# DKT. KIJAZI AELEZA FAIDA KWA NCHI WANACHAMA WA WMO KANDA YA AFRIKA

**Dar es Salaam**




Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) na Makamu wa Tatu wa Rais wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO), Dkt. Agnes Kijazi, ameeleza faida zitakazopatikana kwa Nchi Wanachama wa WMO kanda ya Afrika"WMO Regional Association I – Africa (RA I)"kutokana na uboreshaji wa muundo na majukumu ya kanda za WMO unaotekelezwa na Shirika hilo.

Dkt. Kijazi alieleza hayo tarehe 23 Agosti, 2021 katika mkutano wa 18 wa Nchi Wanachama wa WMO kanda ya Afrika awamu ya pili "Eighteenth Session of WMO Regional Association 1-phase II (RA I – 18(II))",uliofanyika kwa njia ya mtandao kuanzia tarehe 23 hadi 26 Agosti, 2021. Dkt. Kijazi ambaye ni Mwenyekiti wa Kikosi kazi cha WMO cha kufanya mapitio ya muundo na majukumu ya kanda za WMO "(Executive Council Task Force to lead the Comprehensive Review of the WMO Regional Concept and Approaches)", alieleza faida hizo alipowasilisha mada kuhusiana na namna Nchi Wanachama wa WMO kanda ya Afrika zitakavyofaidika na maboreho hayo, ambapo mada hiyo

ililenga kutoa uelewa kuhusiana na manufaa ya maboresho hayo kwa kanda ya Afrika.

Akiwasilisha mada hiyo, Dkt. Kijazi, alisema miongoni mwa faida zitakapatikana kwa Nchi za kanda ya Afrika ni pamoja na kuimarishwa kwa njia za kuibua na kushughulikia vipaumbele vya kanda ya Afrika, ambapo vipaumbele hivyo vitaibuliwa kupitia mfumo maalumu wa WMO (WMO Community Platform). Aidha, maboresho hayo yanatoa fursa kwa viongozi na wataalamu katika kandakujielekeza zaidi katika kujadili na kutoa mapendekezo stahiki ya kutatua changamoto za Nchi Wanachama katika kanda husika. Maboresho hayo pia yataweka mfumo bora wa kuratibu utekelezaji wa maamuzi ya WMO, kwa kuweka utaratibu wa kupima utendaji kazi na utekelezaji wa maamuzi hayo.


Faida zingine ni kuimarika zaidi kwa ushirikiano baina ya Taasisi za Hali ya Hewa, taasisi za maji, sekta binafsi, taasisi za elimu ya juu na mashirika ya Umoja wa Mataifa; Kuimarika na kuongezeka kwa fursa za mashirikiano baina ya Nchi au maeneo yanayohusiana katika kanda; na uboreshwaji wa vituo vya huduma za hali ya hewa vya kikanda (Regional Specialized Meteorological Centres-RSMC) katika kuzijengea uwezo zaidi Nchi Wanachama katika Kanda.

Faida hizo alizoeleza ni sehemu ya mapendekezo ya jopo analoliongoza yatakayowasilishwa na kutolewa maamuzi katika Mkutano Mkuu wa WMO "Extra-Ordinary Meteorological Congress (2021)"unaotarajiwa kufanyika mwezi Oktoba mwaka huu. Mapendekezo hayo yanajumuisha pia majukumu ya Nchi Wanachama katika kanda husika, pamoja na majukumu ya viongozi waandamizi katika kanda. Maboresho hayo ya muundo na majukumu ya kanda za WMO ni mwendelezo wa mabadiliko ya kimfumo yanayotekelezwa na WMO ili kuboresha zaidi huduma za hali ya hewa kwa Nchi Wanachama.

Sambamba na faida zilizoainishwa, mkutano huo pia ulijadili mada mbalimbali, ikiwa ni pamoja na masuala ya uboreshaji wa miundombinu ya hali ya hewa, utafiti na huduma za hali ya hewa barani Afrika. Katika eneo la miundombinu, Mkurugenzi wa Huduma za Utabiri wa TMA, ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya WMO inayoshughulikia uchakataji wa data na utabiri wa hali ya hewa "Standing Committee on Data Processing for Applied Earth System Modeling and Prediction (SC-ESMP)",Dkt. Hamza Kabelwa aliwasilisha mada kuhusu mwongozo wa WMO wa uchakataji wa data na utabiri "Manual on the Global Data Processing and Forecasting System (GDPFS)". Aidha,Mkurugenzi wa Miundombinu na Huduma za Ufundi wa TMA, Dkt. Pascal Waniha alichangia katika mkutabno huo na kushauri Nchi za kanda ya Afrika kuuhuisha mpango wa kuwa na satelaiti ya hali ya hewa ya Afrika itakayosaidia kuboresha upatikanaji wa data za hali ya hewa na hatimaye kuboresha zaidi huduma za hali ya hewa barani Afrika.

## FAHAMU ZAIDI:

### MASUALA MUHIMU YA KUZINGATIA KATIKA UTABIRI WA BAHARINI




**Je ukiona rangi hizi kwenye utabiri wa Baharini zinamaanisha nini?**

| ALAMA | MAELEZO |
|---|---|
| | ◆ Rangi nyeupe inawakilisha upepo tulivu na hali shwari ya bahari |
| | ◆ Rangi ya blue mpauko inawakilisha uwepo wa upepo mdogo na mawimbi madogo baharini |
| | ◆ Rangi ya blue inawakilisha uwepo wa upepo na mawimbi ya wastani baharini |
| | ◆ Rangi ya njano inawakilisha angalizo linalotolewa kuashiria uwezekano wa kutokea upepo mkali na mawimbi makubwa kiasi baharini |
| | ◆ Rangi ya chungwa inawakilisha tahadhari ndogo inayotolewa kuashiria uwezekano wa kutokea kwa upepo mkali na mawimbi makubwa baharini |
| | ◆ Rangi nyekundu inawakilisha tahadhari kubwa inayotolewa kuashiria uwezekano wa kutokea kwa upepo mkali na mawimbi makubwa zaidi baharini |

# KISWAHILI CHETU

## ISTILAHI ZA HALI YA HEWA

Tuangazie herufi H:

| | |
|---|---|
| hail | mvumawe |
| Hailstorm | dhoruba ya mvumawe |
| heat wave | wimbijoto |
| heavy rain | mvua kubwa |
| high pressure system | mfumo wa mgandamizo mkubwa wa hewa |
| high probability | uwezekano mkubwa wa kutokea |
| high tide | bamvua |
| high/strong wind | upepo mkali |
| high yield | mavuno lufufu |
| humidity | unyevuanga |
| hydrology | haidrolojia |
| hygrometer | haigromita |


JARIDA LA MWEZI
TOLEO NA. 007
JULAI, 2021
TMA
1 NAIBU SPIKA: VYOMBO VYA HABARI TENGENI MUDA WA KUTOSHA KURUSHA TAARIFA ZA HALI YA HEWA
2 MAWAZIRI SADC WAPITISHA MAAMUZI KUMI YA SEKTA YA HALI YA HEWA
3 FAHAMU ZAIDI: MASUALA MUHIMU YA KUZINGATIA KATIKA UTABIRI WA HALI MBAYA YA HEWA
ISO 9001: 2015 Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga

**JARIDA HILI LIMEANDALIWA NA:**


**Mhariri**
Monica Mutoni

**Waandishi**
Rehema Maxmin
Wilbert Muruke

**Msanifu Kurasa**
Kennedy Mgeta

**Shukrani**
Ofisi ya Ushirikiano wa Hali ya Hewa Kimataifa
Kituo Kikuu cha Utabiri


www.meteo.go.tz

@tmaservices

@tma_servces

@tanzaniameteorological

www.meteotz1950.blogspot.com

tanzaniametagency

TMAonline TV


Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3,
388 Br. Morogoro
S.L.P 3056,
16102 Dar es Salaam, Tanzania.